

See discussions, stats, and author profiles for this publication at: <https://www.researchgate.net/publication/362304261>

# UJUMBE WA AMANI; KATIKA UCHAGUZI WA 2022 TUKUMBUKE PEEK, PII, PWA, BIYO ZOT<sup>h</sup>E NI L'EAU (MAJI)

Article · July 2022

---

CITATIONS

0

---

READS

71

2 authors, including:



Mohamed Karama

University of Kabianga

14 PUBLICATIONS 2 CITATIONS

SEE PROFILE

Some of the authors of this publication are also working on these related projects:



UCHAMBUZI WA UTENDI WA SIRI LI ASRARI [View project](#)

## UJUMBE WA AMANI

### **KATIKA UCHAGUZI WA 2022 TUKUMBUKE PEEK, PII, PWA, BIYO ZOṬḐE NI L'EAU (MAJI)**

Katika masiku ya hivi karibuni mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali nchini Kenya yamezinruka na kuonya kuhusu barabara wanasiyasa wanayoṭaka kutupeleka huku wakivutiya mikao yao katika Uchaguzi Mkuu unaokuja baada ya muḏa kiḏogo ṭu. Kwa vile kila mwamba ngoma huvutiya kwake, basi, ikawa kumsetḥa mwenziyo ni sawa. Mbiyu za mgambo zilipoanza kufikiriwa kulizwa, Serikali Kḥuu imekuja haraka na kwingiliya kati ili kuweka nidhamu isohaṭarisha amani ya nchi. Haṭuwa hii ya Serikali Kḥuu ni jambo la kupongezwa na kushukuriwa.

Kama wasemavo wazee wetu waṭukufu waloitumikiya nchi hii kwa moyo wao woṭḥe, kura ni wingu la kupitḥa na keshowe kuṭakucha. Naswaha ya neno letu ni kwamba makunri yoṭḥe yaangaliye twaṭoka wapi, tukoje hivi sasa, na kesho twaiṭaraji siku iwe njema vipi.

Tukiyangaliya usawa wa binaḏamu kimaumbo yao, sisi twasema katika mwingiliyano wa lugha zao, piya, hakuna ilo bora kuliko nyengine. Lugha zilizomo Kenya ni nyingi na kila moja ina jukumu la kwenreleza ushikamano na ufungamano ili shabaha na lengo letu liwe moja: kuinuwa Kenya kihali na kimali. AMANI BAINA YA JAMII ZETU IMO KATIKA KILA KITḐU kama tuṭakavoonesha hapa chini.

Mfano mmoja tulouchaguwa sisi kwangaziya mwingiliyano huu ni neno ṭukufu lenye kunasibishwa na uhai wa mwanḏamu kokotḥe aliko ulimwenguni. Yasemwa maji ni uhai. Kila lugha katika ulimwengu lazima inalo neno hili la kimsingi katika hazina ya misamiyaṭi yake. Maneno:

peek	–	kiKalenjin
pii	–	kiJaluo
biyo	–	kiKushiti
pani	–	kiHindi
pwa	–	kiSwahili lahaja
maji	–	kiSwahili Sanifu

yoṭḥe yamaanisha maa (kiArabu), l'eau (hutamkwa 'lu') (kiFaransa). Tukiyangaliya kwa makini maneno yoṭḥe yaliyoorodheshwa yana sauṭi /p/, /b/ na /m/. Twaweza kusema asili yao ni moja kwa kuwa zoṭḥe ni sauṭi za miḏomoni na yanamaanisha 'maji'.

Katika kiSwahili 'pwani' ni mgawanyiko wa mofimu mbili /pwa- + -ni/. /-ni/ ni kiyelezi cha mahali. Waswahili wa Mambasa husema "kwenra baharini" na Waamu hunena, "kwenra pwani" kwa maana ya 'kwenra kwenye yale maji'. Kwa hivyo, /pwa-/ ina maana ya 'maji'. Hata Shihabudin Chiraghdin katika *Historia ya Kiswahili* (1977) amelitumiya neno hili 'pwa' kwa maana ya 'mwambao'. Hali kadhalika, bingwa mmoja wa kiSwahili alitwambia kuwa 'mluo' ni kiSwahili cha kale linaloamaanisha 'mto', hivyo basi, dhana ya

maji i palepale. Yaweza kuwa piya ‘mluwo’ ni ukopaji kutoka lugha za kiRumi (kiFaransa katika mfano hapo juu). Kutokana na mfanano huu lugha zetu zatwambiya nini? Tukaye tu tafakari kuwa maingiliyano yetu ni ya tangu jadi haṭa lugha zetu piya zasema hivo.

Kwa mintarafu ya mshikamano wa maneno yetu, vilevile, mwenenro wetu katika jambo hili la Uchaguzi Mkuu 2022 liwe ni la amani, utangamano na upendo katika nchi yetu. Hapana shaka tarehe 10 Agosti juwa litakucha tutake tusitake; imani yetu kutapambauka katika mafungamano ya kheri. **KAMA YALIVYO MAJI NI UHAI NA AMANI NI VIVYO!**

Mohamed Karama & Alexander Rotich  
University of Kabianga  
Kericho, Kenya.